**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KIDATO CHA TATU**

**KISWAHILI (INSHA)**

**KARATASI YA 1**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1. Barua rasmi**

- Barua hii iwe na anwani mbili
- Iwe na tarehe
- Mtajo
- Mada – iandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari
- Utangulizi – historia fupi kumhusu – mwomba kazi
- Aonyeshe lengo la kuomba kazi
- Aeleze elimu yake, tajriba yake, ufaafu wake
- Barua hii iwe na sura ya barua rasmi
- Mwili (katika aya mbali mbali)

**Wasifu kazi**

Maelezo ya kibinafsi

- Jina

Tarehe na mahali pa kuzaliwa

Ndoa

Anwani

Uana

Simu

**Maelezo ya kielimu**

Chuo kikuu

Shule ya sekondari

Shule ya msingi

(Shule ulizosomea, mitihani uliyofanya na vyeti

Tajriba – kazi ulizowahi kufanya, vyeo na muda

**Uraibu**

1.

2.

**Maandisha na machapisho**

Uanachama

1.

2.

**Warejelewa**

1. Jina / Anwani

2. Jina / Anwani

Mwanafunzi azingatie vichwa vidogo vidogo

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Makosa ya sarufi, hijai na mtindo yaandhibiwe

**2.** Serikali yafaa kufanya yafuatayo

1. Kuongeza idadi ya walinda usalama
2. Walinda usalama kupewa silaha za kisasa
3. Walinda usalama kupewa vyombo vya usafiri vya kutosha kama vile motaboti, ndege, magari n.k.
4. Ulinzi kuimarishwa forodhani, vituo vya magari na katika viwanja vya ndege.
5. Walinzi kuongezwa na kuimarishwa mipakani.
6. Misako kufanywa ili kunasa walio nchini kinyume cha sheria
7. Misako kufanywa ili kuwapokonya raia silaha.
8. Raia kushirikishwa katika kuimarisha usalama.
9. Hatua kali za kisheria dhidi ya aina yoyote ya uhalifu.
10. Vikosi vya usalama kupewa mafunzo maalum
11. Kuanzishwa kwa vikosi maalum vya kukabili magaidi.
12. Serikali kushirikiana nanchi jirani katika vita dhidi ya ugaidi wa kimataifa.
13. Vikundi haramu nchini kukabiliwa na serikali kisheria na kijeshi.
14. Serikali kutoa tuzo kwa wanaotoa habari muhimu za kuwezesha wahalifu kutiwa nguvuni

**3.** Hii ni insha ya methali

- Maana yake: Mtu mwenye subira hatimaye huona raha. Km; atakayesubiri tunda lililovumbikwa atalila likiwa bivu.
- Matumizi; methali hii hutumiwa kumliwaza na kumfariji mtu anayekumbana na shida kumhimiza asubiri hadi mwisho; atakapofanikiwa.
- Mtahiniwa abuni kisa kinachothibitisha ukweli wa methali hii.
- Kisa kiangazie sehemu mbili km:

i) Mhusika atakayevumilia shida / madhila

ii) Na vile mhusika Yule ataishia kufanikiwa

Tanbihi: mtahiniwa akionyesha upande mmoja apate chini ya 10/20.

**4.** Insha ya mdokezo

Mtahiniwa aandike kisa kitakachoonyesha majuto baada ya kujipata taabani. Hii iwe baada ya maelekezo kutoka kwa mwalimu mkuu; yaliyoambulia patupu.

**Au**

Mwanafunzi aandike kisa kitakachoonyesha furaha baada ya kufuata ushauri wa mwalimu mkuu. Ushindi wake usababishe furaha isiyo na kifani inayoambatana na kilio na machozi ya furaha.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes